

Jina.....

Nambari.....

Shule.....

Sahihi.....

Tarehe.....

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2

LUGHA

JULAI/ AGOSTI

Muda : Saa 2 ½

**MTIHANI YA PAMOJA WA WILAYA YA MANGA -2012
CHETI CHA KUHITIMU ELIMU YA SHULE YA UPILE**

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2

LUGHA

JULAI/ AGOSTI

Muda :Saa 2 ½

Maagizo:

1. **Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachwa hapo juu.**
2. **Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.**
3. **Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.**
4. **Mtihani una alama 80.**

Kwa matukizi yamtihani pekee.

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	80	

Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa

Watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa

Soma kifungu kifuatacho kaisha ujibu maswali.

Hadhari kabla ya hatari au athari, ni usemi ambao sikupata kuelewa maana yake hadi nilipofika mjini Kigali, mji mkuu wa Rwanda. Sikufika pale kwa sababu ya kuhajiri nchi yangu; ilikuwa ziara ya kutaka kubadili mazingira na kufariji mtima wangu.

Dimba ya kupanga safari ya kuzuru Rwanda, ilichukua muda mrefu kupanga na kulihitajika kiasi kikubwa cha dirhamu, kugharamia mahitaji yote ya safari. Wahisani bora, maswahibu na wafanyakazi wenzangu, walichanga bia kwa nia ya kutaka kweli, nisikose kutimiza malengo yangu. Yumkini, walijua fika kuwa, marajeo yangu, yangewaondolea parandesi, mambo mengi yaliyokuwa yakiwazuga akili kwa kutofafanuliwa vizuri. Wazo kwamba, watu wa Rwanda wanaishi kama ndugu wa toka nitoke, hawataki kukumbushwa mauja yaliyosababisha mauaji ya watu zaidi ya milioni moja.

Basi lilitotubeba lilipitia nchi ya Kenya, ambapo tulishuhudia mambo mengi tangu tuvuke mpaka kupitia Namanga hadi kuingia taifa la Uganda kwa kuvuka mpaka wa Busia. Kilimo kilikuwa kimestawishwa, miti mingi ya kila nui ilibingirisha matawi yaliyosifia mvua ya masika, raia wengi walionekana kuwa na haraka za kwenda walikochelewa, huku wachache wakionekana wamezembea barabaran, bila kutia gange ya ama yoyote.

Siku mbili nchini Uganda zilitosha kushuhudia heshima ya ajabu wapatayo waume wa kule. Wanawake wamejifunza kuzungumza kwa matao ya chini, magoti yao yakiumia mchangani kwa kutotaka wasionekane watovu wa mila. Mapishi yao ni ya kutaka urudi tena kuwasalimia. Raia wengi huzungumza kwa utaratibu wa kufikiriwa kuwa wao ni wanyonge, lakini walisemalo ndilo liwalo. Ajabu ya kutisha ni kwamba kila kitu hununuliwa kwa maelfu. Sharti mtu awe na kapu kubwa la noti, ikiwa ataotea unununuzi wa chochote cha kusifikika.

Kungia Rwanda ni ngoma ghaya katika mpaka wake na Uganda. Uchunguzi wa kina ulifanywa, na askari ambao wanaelewa maana hasa ya neno usalama.

Ukitaka kujua ubora wa mu wa Kigali, fika usiku. Tuliyoona si mambo ya kutofika toka akilini kwa urahisi. Siraji zilikuwa zinawaka kila upembe, mtaa na jengo. Mchana wao, umejaa bidii utu, heshima, hifadhi ya mazingira na nyimbo za kuhimiza umoja wa taifa lao. Kila kona ma maandishi makubwa ya kuonyesha kuwa wanaadhimisha miaka 18 tangu mauaji ya kutisha ulimwengu yatokee, mauaji yaliyochochewa na ukabila. Raia wao kama kiongozi hadi mtoto wa kujifunza kuongea, wana lengo moja; kupendana, kuisaidiana, kusameheana na kujenga taifa la kabila moja. Adui wao mkubwa ni anayewakumbusha walikotoka.

Maswali.

(a) Onyesha malengo mawili yaliyoguswa katika taarifa. (al.2)

(i)

(ii)

(b) Taja tofauti moja ya wazi baina ya watu wa Kenya na watu wa Rwanda. (al.2)

.....

.....

(c) Unafiki ni kwa nini watu wa Rwanda wana hamu ya kusahau yaliyopita? (al.2)

(i)

(ii)

(d) Makala uliyosoma yanatoa funzo gani kuhusu taifa linalotaka kustawi? (al.4)

(i)

(ii)

(iii)

(iv)

(e) Msimulizi alichukua muda gani kufika Rwanda? (al.1)

.....

.....

(f) Eleza maana ya maneno haya katika muktadha wa matumizi yao: (al.4)

i) mauja

.....

.....

ii) dimba

.....

.....

iii) maswahibu

.....

.....

iv) yumkini

.....

.....

2. MUHTASARI

(ALAMA 15)

Soma kifungu hiki kasha jibu maswali yafuatayo.

Ujana hauna mipaka kamili. Ni hali ya watoto na utu wa makamo. Jamii mbalimbali zinakadiria ujana kwa vipimo mbalimbali. Kwa madhumuni ya kifungu hiki tutaugawanya ujana katika vipindi viwili.

Katika kipindi cha kwanza kuna mabadiliko ya kimwili na ya kiakili. Mull ya vijana inabadilika kutoka utotoni hadi utu uzima. Wasichana huvunja ungo. Umbo hubadilika, ukadhihiri urembo kama malaika. Nao huringa kama fausi. Lugha ya hujaa msamiati wa mapambo, mitindo ya mavazi na wa mapenzi. Hujikwatua kwatukwatu na kujipodoa podopodo. Wanajigeuza windo jepesi kwa wawindaji waliotapakaa kotekote.

Wavulana hubaleghe kwa kubadilika sauti zao; zikawa nzito kiasi.

Ni wakati mgumu kwao kwani kwa wengi sauti zenyewe hukirihi na kujaa mikwaruzo ya kuwaaibisha. Huu ni wakati ambao vijana engi huweka mipaka baina ya na ulimwengu kwa ujumla. Wana matumaini, matarajio na mahitaji chungu nzima. Wao hujiona bora zaidi kimawazo. Wanataka kujaribisha kila kitu-chema au kibaya. Wasichana hupendelea kuvaa mavazi ya kiume. Wavulana nao hutoga masikio au sikio moja tu! Huvaa herini na mikufu na hata kusuka nywele.

Ni wakati wa mkengeuko. Huiga mambo bila kuchuja; huwa wepesi wa hasira na harara wa uamuzi. Wengi hushiriki uvivu wakatimia muda mwingi kulaza damu na kupendelea kulala au kutazama runinga na video. Wanapendelea muziki wa rabsha ambao unaweza kumwamsha alalaye kaburi. Hapo ndipo tena wanaingilia uvutaji wa sigara au bangi, dawa za kuievya, ulevi, uasherati na kukiuka maadili. Kuna hatari kubwa ya kuambukizwa ukimwi na magonjwa mengine. Wana mambo mengi ya kujidhulumu wenyewe. Haja kwao ni kupencjwa, kutambuliwa na kukubaliwa na marafiki, tosha!

Punde si punde kipindi cha pill cha ujana hufika . Wengi hugutuka kwa jinsi walivyopitikiwa wa wakati na huwa wamemaliza masomo au kuacha shule. Hawamthamini mzazi wala mwalimu wao. Baadhi yao sasa wana kazi na pato lao wenyewe . Idadi fulani wanajikuta kwenye janga la kuwa mzazi wa pekee bila mwenzake wa kumsaidia. Wanayajutia sana matendo yao ya awali na wanaweza kupigiwa mfano kuwa ,maji yakimwagika hayazoleki.

Kufumba na kufumbua kijana wa juzi sasa ni mzazi wa vijana . Yeye hawaelewi wala nao hawamsikizi. Kweli ujana ni moshi. Ni muhimu kuingia vuguvugu hill kwa uangalifu. Wazazi, walimu, jamli na hata serikali ma jukumu la kuwaelekeza na pia kuwasaidia vijana kuvuka daraja hill legevu.

3. MATUMIZI YA LUGHA

(ALAMA 40)

(a) Tunga sentensi moja ukitumia

(al.2)

(i) Kivumishi cha kumiliki

.....

(ii) Kiwakilishi kirejeshi cha nafsi

.....

(b) Sahihisha

(i) Gari likubwa imepakwa rangi

.....

(ii) Ukiwa mnono sana unaweza kusirai

(al.2)

.....

(c) Taja sauti:

(i) Mbili za menoni..... na.....

(ii) Mbili za kooni..... na..... (al.2)

(d) Onyesha matumizi mawili ya 'Herufi za mlazo'

(i)

.....

(ii)

.....

(e) Dhihirisha matumizi ya vitate vifuatavyo katika sentensi moja moja

(i) Chea/shehe

.....

(ii) Che/je

.....

(f) Bainisha matumizi ya ndi- katika sentensi zifuatazo:

(al.2)

(i) Ninyi ndinyi mnaotafutwa na polisi

.....

(ii) Tumbo lake ndilo linalonguruma

.....

(g) Akifisha

Rwanda ni nchi iliyotawaliwa na wafaransa na si waingereza Somalia ingawa inaendelea

kuhangaishwa haijulikani ilitawaliwa na nani

(al.3)

.....

.....

.....

(h) Andika katika usemi wa taarifa
'Masoma ya ziada,yataendelea leo,kasha na hadi tumalize muhula huu.Ikiwa kuna wa kupiga
aseme sasa kabla sijaondoka hapa.'Mwalimu alisema. (al.4)

(i) Tambua mofimu mzizi na mofimu nyambulishi katika fungutenzi: (al.2)

(i) sahauliwa

(ii) andikishwa

(j) Kwa vielelezo vya vishale au mistari,changanua sentensi hii. (al.4)

Mtu mmoja mrefu alipatikana baada ya wizi

(k) (i) Tunga sentensi moja inayoonyesha matumizi ya nomino yoyote ambatano (al.2)

(ii) Kanusha sentensi hii

Akija an atake kuzungumza umwadhibu (al.2)

(iii) Yakinisha

Sikudhani wala kupata kuwa asiyekuwako na lake haliko. (al.2)

(iv) Weka katika wastani wingi

Jiji la jizi hatari ni hili (al.2)

(l) Kipi kivai na kipi kishazi katika sentensi hii?

Mkulima yule mrefu amepanda mihogo (al.2)

(m) Unda sentasi moja badala ya: (al.3)

(i) Osama aliuliwa na majasusi waledi

(ii) Osama alikuwa amejificha karibu na kambi ya jeshi.

(iii) Majasusi walipanga kumuua Osama kwa muda wa miezi sita mtawalia.

4. ISIMU JAMII

(ALAMA 10)

(a) Ni sifa gani hubainisha sajihi ya bashara

(i)

.....

(ii)

.....

(iii)

.....

(iv)

.....

(v)

.....

(b) Onyesha mambo yanayofanya lugha fulani kukua

(i)

.....

(ii)

.....

(iii)

.....

(iv)

.....

(v)

.....